**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**
**BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA**

## TANGAZO KWA UMMA

## MAFUNZO KWA WAFANYAKAZI WATAKAOHUDUMU KWENYE GHALA KUU MSIMU WA ZAO LA KOROSHO 2026/2027

Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) ni Taasisi chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara iliyoundwa kwa **Sheria ya Stakabadhi za Ghala Sura 339.** Bodi pamoja na mambo mengine imepewa jukumu la kutoa leseni kwa Waendesha Ghala, Meneja Dhamana na Wakaguzi wa Ghala.

Bodi inapenda kuutaarifu umma kuwa itaendesha mafunzo maalumu kwa wafanyakazi watakaohudumu kwenye ghala mbalimbali kuelekea **msimu wa 2026/2027 wa mauzo ya zao la korosho** kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

Lengo la mafunzo haya ni kuwaongezea washiriki uelewa kuhusu Mfumo wa Stakabadhi za Ghala, mahitaji ya uzingatiaji wa kanuni na sheria, usimamizi wa hatari, viwango vya uendeshaji pamoja na mbinu bora za usimamizi wa bidhaa.

Mafunzo haya yanatarajiwa kufanyika **Mkoani Mtwara tarehe 14 hadi 19 Septemba 2026 katika ukumbi wa Tiffany Hotel.** Gharama za mafunzo ni **Shilingi Laki Saba na Elfu Hamsini Tu (Sh. 750,000).** Gharama hii imejumuisha chakula (asubuhi na mchana), shajala pamoja na vyeti kwa watakaofaulu mtihani wa Bodi.

Washiriki wenye nia wanatakiwa kujisajili pamoja na kufanya malipo kabla ya **tarehe 11 Septemba 2026.**

Kwa usajili na kupata bili ya malipo *(control number)* tafadhali tumia *link* hii hapa http://41.59.85.9/. Kwa maelezo zaidi, wasiliana na **Bi. Rosemary Samson** kwa simu namba **0753 408 769** au barua pepe **rosemary.samson@wrrb.go.tz** au **Bw. Edward Kafuka** kwa simu namba **0767 828 365** au barua pepe **edward.kafuka@wrrb.go.tz.**

***NB:** Washiriki wanaombwa kuja na tarakilishi mpakato (laptop) kwa ajili ya kuwezesha mafunzo ya mifumo ya tehama ya Bodi.*

Imetolewa na;

**MKURUGENZI MTENDAJI**
**24 AGOSTI 2026**